



ilometa opitika

ina kilometa 849.42
hizo kilometa
ngarawe na kilo-
umi.
le wa barabara
lometa 1,221.81
huo wa barabara
l ni lami wakati
ni za changarawe,"

ndao wa barabara
kiwamo Daraja
alo ni kiungo
oa wa Morogoro
ya Tanzania.
aye alikuwa
waandishi wa
tilia maendeleo na
ira mkoani hapa
ndaji Mkuu wa
red Besta, alisema
u ya Sita imeaz-
izi makubwa kati
barabara.

'Serikali haitawavumilia wafugaji wakorofi'

Na John Nditi, Mvomero

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imesema haitawaunga mkono wafugaji wakorofi na wasiofuata sheria zinazosimamia matumizi bora ya ardhi.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Alexander Mnyeti alisema haitawaunga mkono watako-sababisha migogoro baina yao na watumiaji wengine wa ardhi wakiwamo wakulima.

Alisema hayo hivi karibuni wilayani Mvomero kwenye uzindu-uzi wa kampeni ya Tutunzane. Mvomero 2023 iliyoizinduliwa na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima.

Mnyeti alisema baadhi ya wafugaji wamekuwa wakitumia uwezo wao wa kifedha kutoa rushwa kwa baadhi ya watoa maamuzi wanapofikishwa kwenye vyombo vya haki, licha ya mkulima kupata hasara ya mazao yake kuliwa mifugo, huonekana ndiye mkosaji na kushindwa kupata haki yake.

"Wizara ya Mifugo na Uvuvi tumeamua kusimamia ukweli na sheria, hatutakuwa tayari kumtetea mfugaji atakayevunja sheria na kuingiza mifugo kwenye mashamba ya wakulima kwani kumtetea ni kuchochea migogoro ndani ya Wilaya ya Mvomero na maeneo mengine nchini," alisema.

Pamoja na hayo, aliwataka wafugaji wa Wilaya ya Mvomero na nyingine ndani ya mkoa huo, kuanza kufuga mifugo yenye tija kwa taifa na kujiepusha kutumia fedha walizonazo kuwanyanyasa wakulima.

45>>Idadi ya watoto

UHURU UK 8
 * TAFIRI, FAO wageukia * JK
 utafiti rasilimali uvuvi u

Na MWANDISHI WETU

TAASISI ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI), Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) na Chuo Kikuu Cha DUKE cha Marekani, zinafanya utafiti kufahamu na kupata taarifa sahihi ya rasilimali za uvuvi zilizopo nchini.

Akizungumza katika warsha jijini Dar es Salaam, Kaimu Mkurugenzi Idara ya Uvuvi kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Stephen Lukanga, alisema tafiti hizo zitaibua taarifa za maeneo ambayo sehemu ya maziwa na Bahari ya Hindi.

Lukanga alisema idadi ya watu nchini imeongezeka na kufikia zaidi ya milioni 60 lakini taarifa zilizopo zinatolewa kulingana na idadi ya zamani ya zaidi ya milioni 40, ambayo imekuwa ikibainisha watu wanaojishughulisha katika sekta ya uvuvi ni milioni 4.5.

"Warsha hii ilianzishwa na wanasayansi, watafiti kutoka nchi zaidi ya 58 kuhakikisha rasilimali ambazo hazijonyeshi zionekana, hususan uvuvi mdogo kuongeza pato la taifa".

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi wa Maendeleo ya Utafiti na Uratibu wa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) Dk. Mary Kishe, alisema taasisi hiyo ambayo mwaka huu inafikisha miaka 40, imekuwa ikikusanya na kutafiti masuala ya sekta ya uvuvi.

Alisema TAFIRI inashirikiana na FAO, Chuo Kikuu Cha DUKE wataunganisha taarifa za zamani na kuziweka pamoja na kuona umuhimu wa takwimu hizo kwa maendeleo endelevu ya sekta ya uvuvi.

Pia alisema warsha hiyo ni muhimu ambapo watafiti watapata fursa ya kutoa mapendekezo ya namna ya kusimamia rasilimali za uvuvi, kufikia lengo la sekta hiyo kuongeza mchango katika pato la taifa.

Kwa upande wake Ofisa Mkuu wa FAO, Nicolas Gutierrez, na Ofisa Mipango Mtafiti kutoka FAO Nicole Franz, walisema uwepo wa taarifa sahihi ni muhimu katika kuendeleza sekta ya uvuvi nchini na kutoa elimu kwa wavuvi.